



Mkataba wa Tamaduni Mbalimbali Katika Australia ya Kusini

Sheria ya Tamaduni nyingi ya Australia Kusini ya 2021 inaweka lengo la kuendeleza tamaduni nyingi na ushirikiano wa kitamaduni na inatoa Mkataba wa Tamaduni Mbalimbali wa Australia Kusini (Mkataba). Mkataba huu utatoa maono na mwongozo kwa mashirika ya Australia Kusini, mashirika, taasisi, biashara na jumuiya kama msingi wa maendeleo ya sera za Australia Kusini na muundo na utoaji wa huduma zao.

Mkataba wa Tamaduni mbalimbali wa Australia ya Kusini unakubali:

- Watu wa asili (Aboriginal) kama Wamiliki wa Jadi na wakaaji wa ardhi na maji katika Australia ya Kusini ambao wanaendelea kudumisha na kukuza imani zao za kitamaduni na urithi kama tamaduni tofauti zilizoishi kwa muda mrefu zaidi, na jukumu muhimu la kihistoria na linaloendelea kama watu wa Mataifa ya Kwanza katika Australia Kusini.
- Mafanikio na changamoto za vizazi vilivyokuja kabla yetu na ambao, pamoja na jumuiya mpya na zinazoibukia, husaidia kuunda utambulisho wa Australia Kusini.

Mkataba huu ni wa Waaustralia ya Kusini wote na unalenga:

- uunganisha jamii yetu kwa kutambua tofauti za kitamaduni, lugha, rangi na dini.
- kuunda mazingira ambayo tunaweza kueleza, kubadilishana maarifa, mawazo na mitazamo kikamilifu ili Waaustralia ya Kusini wote wawe na uelewa wa kina na heshima kwa utajiri na thamani ya utofauti wetu.
- kutoa msingi wa maendeleo ya sera za tamaduni nyingi na utoaji wa huduma ambazo zitanufaisha jamii zetu na kusababisha maendeleo ya Jimbo letu.
- kuhimiza sehemu za kazi zinazojumuika na zinazowajibika na jumuiya kwa Waaustralia ya Kusini wote.

Honourable Peter Malinauskas MP
Premier of South Australia

Honourable Zoe Bettison MP
Minister for Multicultural Affairs

Damien Walker
Chief Executive
Department of the Premier and Cabinet



Kanuni za Mkataba

Mkataba wa Tamaduni
Mbalimbali wa Australia ya
Kusini unaweka kanuni ambazo kwazo
Waaustralia ya Kusini wote:

1. Kutambua, kuheshimu na kuthamini tofauti za kitamaduni, lugha, rangi na dini na mchango ambao hili limetoa na linaendelea kutoa kwa Jimbo letu.
2. Wanahimizwa kushiriki katika kubadilishana maarifa na kuelewa tofauti zetu za kitamaduni, lugha, rangi na kidini.
3. Wana uwezo wa kuishi, kufanya kazi na kusoma ili kustawi katika nyanja zote za maisha katika jamii yenyе mshikamano.
4. Wana haki ya kuheshimiana, kuelewana, haki, usalama na uhuru dhidi ya kubaguliwa kwa misingi ya utamaduni, lugha, rangi na dini zao.
5. Wanapaswa kuwa na uwezo wa kuhifadhi, kueleza, kutekeleza na kusherehekea tofauti zao za kitamaduni, lugha na kidini.
6. Kuwa na ufikiaji sawa wa fursa na huduma zinazosaidia ushiriki katika maisha ya kielimu, kijamii, kitamaduni, kiuchumi na kisiasa ya Jimbo letu.